# Gazeti la Kimataifa
## Waabuduo Damu ya Kristo

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma


www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org


...Kwa Neno Lako...

Lima, Peru 5-28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 12, Novemba 2018


Mhariri

## Heri ya utakatifu

Kila mbatizwa amepokea zawadi hii: utakatifu. Ni wajibu ambao hautufanyi watumwa na wala kutuondolea nguvu, bali unatupa uhuru, furaha na amani. Haututoi nje ya ulimwengu, hautufungii ndani wala kutufunga kwenye ubinafsi wetu kama kwenye kisiwa chenye furaha, ni utume ambao tumekabidhiwa, ambao unatupelekea kukutana na hali halisi ya ulimwengu na kuwenda zaidi ya akili ambazo mara nyingi hutaka kutueleza yote ya Mungu au kuamini, mbali na matakwa yetu na nguvu zetu, kwamba daima yupo Mungu ambaye anatuzawadia huruma yake. Madhaifu yetu ni zana za thamani ili Mungu ajifunue kwetu.

Katika umasikini na kilio, siishi kwa kukata tamaa, bali kwa furaha; ninapokutana na mtu anayelala njiani, mpakani, kijana aliyechanganyikiwa, sithani kwamba ni kizuizi au tatizo la kutatuliwa na wengine, bali kwa mwanga wa imani ninatambua heshima yake kama mtu, aliyekombolewa kwa Damu ya Kristo. Sibaki katika kutokujali au katika kutuma, bali najiachia kuchochewa na kuhojiwa. Utakatifu ni uhusiano wa karibu na Bwana ambao unanifanya nipokee na kukabiliana na matatizo ya sasa ya ulimwengu wa leo, kama uhamiaji. Kwa upole na unyenyekevu, ninasukumwa nje yangu na nje ya mahitaji yangu, nikiamini kuwa tatizo la mwingine ni kubwa kuliko langu.

Tunaitwa kwa ujasiri kutoa majibu ya changamoto za wakati wetu, kuchafua mikono yetu ili kuwa wajenzi wa ubinadamu, ili uwe na ladha ya heri; kuwa wanaume na wanawake wa siku zijazo, ambao wanabubujika asubuhi mpya, waleta matumaini ya maisha yenye kupambwa kwa upendo na huruma ya Mungu.



**Sr. Mimma Scalera, ASC**

## Mhutasari


*Mhariri*
- Heri ya Utakatifu 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*
- Guinea…nchi ya kupenda 2
- Jumuiya ya Kimataifa ya Malezi ya Novisiati 4

*Toka Ulimwengu ASC*
- Yaliyomo sasa Liberia 5
- Semina: Maisha ya Jumuiya ASC 6
- Wanafunzi wa Shule ya Damu Azizi 7
- Kumkumbuka Rudy Torrini 8
- Sisi ni “kijiji” ni haki kulea watoto 9
- …Ndani ya nchi ya Argentina 10
- Majira ya uchambuzi 10
- Kugusa madonda ya Yesu 11

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*
- Kusherehekea Kipindi cha Uumbaji kwa mtindo wa ASC 12

*Ndani ya Shirika*
- Kalenda ya Uongozi Mkuu 14
- Sikukuu za kuzaliwa: tunasherehekea maisha 14
- Waliorudi Nyumbani kwa Baba 14

## Guinea ... nchi ya kupenda

Guinea Bissau imekuwa daima mahali ambapo nilitamani kutembelea: nchi ambayo siku zote niliiona "mbali sana na na upeo wa macho", mbali sana na maslahi ya ulimwengu "uliostaarabika". Ni nchi inayoahidi uzazi, ambayo inaonyesha ukarimu na si chuki, lakini ambapo watu bado wanaishi bila mahitaji ya lazima na mara nyingi katika hali ya umaskini mkubwa. Ni nchi yenye utajiri wa mapambano kati ya maisha na kifo, ya furaha na mateso, ya uzazi na njaa. Kile



kinachobakia ndani ya moyo ni kwamba, licha ya shida nyingi ambazo wanapaswa kukabiliana nazo kila siku, watu daima wana sababu ya kuimba, kutabasamu, kucheza na kutumaini. Ni furaha ya maskini!

Nataka kuwashirikisha mawazo na hisia kadhaa nilizopata katika kipindi nilichoishi na masista wa Foundation ya Guinea ambazo zilitiwa alama kwa baraka na furaha ya ndani ya kukaa pamoja. Zilikuwa siku muhimu, kila kitu kwangu kilikuwa kipya na hivyo nilitafuta namna ya kuishi kwa umakini na uangalifu, nikiacha kila kitu kipate mapokezi ndani mwangu.

Ukweli mara moja ulionekana kuwa changamoto kubwa .. ulimwengu mwingine, utamaduni mwingine wa kupokea na ambao unakuacha uinjilishwe.

Guinea ni nchi maalum, vigumu kuelezea! Kuna maeneo ambayo yanaiba moyo wako na kukuingiza kwenye ndoto. Bissau, Ingorè na Bula ... safari isiyoweza kusahaulika, miongoni mwa nyuso, rangi, mandhari zisizochafuliwa na zenye tamaa kubwa ya kukombolewa. Idadi ya watu wa Guinea Bissau ni wakazi milioni moja na nusu wakiwa chini ya makabila thelathini tofauti. Nchi inakabiliwa na hali ya kutokuwa na utulivu wa kisiasa na usalama wa kijamii, ambayo huongeza umasikini. Kama ilivyo katika sehemu nyingine za Afrika, wanawake hufanya kazi nyingi ambazo huziwezesha familia kuishi na asilimia ya watoto wagonjwa na walio na utapia mlo ni ya juu sana; janga la kweli la kijamii ... matokeo ya mifumo yetu ya kisiasa na kiuchumi inayokuza utengano mkubwa daima kati ya masikini na matajiri.

Matukio ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na kutojali maslahi ya umma yamesababisha kutokuaminiana na uchovu kwa watu. Kanisa linafanya kazi kwa ajili ya kujenga maadili na ustaarabu wa maisha ya kidemokrasia ya nchi na kuishi maisha ya kijamii kwa ajili ya wananchi.

Wazo langu linasimama mara moja kwenye safari ya kurudi Ingorè.sehemu unayopita kati nafasi safi na sehemu za upeo wa macho zinazong'ara! Mchanganyiko wa anga, udongo, uoto wa asili ulio wa kijani, na kubaki ukiufurahia. Ndivyo ulimwengu wa Kiafrika ulivyojitambulisha katika umaskini ulioheshimika mbele ya macho yangu na kunivutia!





Siku zilipita haraka kati ya ziara, mikutano na matukio ya kusherehekea! Tarehe 15 Septemba, sikukuu ya Maria, Mwanamke wa Agano Jipya, tuliishi siku iliyojaa matukio: asubuhi, kuanza hatua ya unovisi Diana na Ludimila, na kwenye adhimisho la Misa mchana nadhiri za kwanza za Sr. Vittoria, Sr. Bighada na Sr. Tania na kurudia nadhiri Sr. Fatima, Sr. Lazara na Sr. Numò. Foundation inaendelea kukua: wanawake kadhaa wanatamani kumfuata Bwana kupitia nyayo zilizoachwa na Mtakatifu Maria De Mattias. Malezi ya mwanzo na endelevu yanapewa kipaumbele na yanapata uhai mkubwa wa kimisionari.
Wakati wa mkutano huko Bula pamoja na masista wote wa Foundation, niliweza kutambua umakini ambao hutolewa katika maisha ya jumuiya kama nafasi ya kutano takatifu katika kuunganisha mahusiano ya kiinjili ambayo ni ushuhuda na unabii.
Haukukosekana muda wa kutembelea jumuiya na maeneo ambapo masista hufanya kazi zao za kiutume ambazo zinahusiana na elimu, kusoma na maendeleo ya kibinadamu. Kuna mahitaji ya watu: ya haraka, hasa chakula na afya, ni utaratibu wa siku na jitihada kubwa ili kuchagua uzima. Ni ujasiri kiasi gani, ni shauku iliyoje ... moto wa mwanzo!
Ilikuwa ni maumivu tuliposimama kwenye kaburi la Sr Romana na Sr. Esperia, ili kusikiliza masimulizi ya 18 Juni 2016, wakati maisha yalipoonekana kukatika mbele ya tukio hilo chungu na lisilotazamiwa.
Ninaangalia tena uso wa kila sista na ninamtukuza Bwana kwa sababu ameweka ndani ya moyo wa kila mmoja shauku kubwa ya "kuwa upendo". Ninamshukuru kila sista wa Foundation kwa umakini na upendo kwa kunikaribisha mimi. Kila mmoja ni zawadi ya pekee, ya thamani na isiyoweza kujirudia kwa ajili ya Shirika na kwa ajili ya ulimwengu.
Maisha yaliyotolewa ya hawa masista ni baraka kwetu sisi sote; kwa kuyatumia kwa ajili ya Ufalme ni ushuhuda muhimu sana wa kile tunachoitwa kuwa "ushuhuda wa kuaminika zaidi wa upendo mwanana wa Mungu, ambao Damu ya Yesu ni ishara yenye ufasaha na ahadi ya agano la milele" (CdV 2).
Guinea iliingia ndani ya moyo wangu hata kabla ya kuwa machoni pangu, ilinifanya nitembee katika ndoto hata kabla ya kutembelea nchi yenyewe. Imenifanya nitambue kwamba utajiri wa watu masikini ni katika roho, hung'ara kama almasi ndani ya mioyo yao, huakisi mwanga, hata mwanga mkali ambao huangaza nyuso zao za tabasamu elfu.
Ni kweli, kuondoka inamaanisha kuthubutu... kurudi haiwi tena sawa na mwanzo.

***Sr. Nadia Coppa, ASC***



# Jumuiya ya kimataifa ya malezi ya novisiati

Kuanzia tarehe 5 hadi 7 Oktoba, kwenye Nyumba Kuu ya ASC Roma ilianza safari ya malezi ya jumuiya mpya ya mchanganyiko wa tamaduni, ile ya novisiati ya kimataifa ya Shirika.

Jumuiya ya malezi ya novisiati ya kimataifa, iliyoitwa hivi karibuni, ilikutana ili kuanza mwaka wa maandalizi, katika kusubiri kupokea wanovisi mwezi Novemba 2019. Mada ilikuwa: “Wanawake waliowekwa wakfu katika Damu ya Kristo/ Wito wetu katika Kanisa”.

Wakati wa sala ya masifu ya jioni siku ya Ijumaa, jumuiya mpya ilipokea baraka na baadaye utambulisho ulifanyka wakati wa chakula cha usiku, timu hii ilianza mashirikisho ya historia na tafakari juu ya Wito, kwa mtazamo wa kibiblia, maendeleo ya kiutu na kwa matazamio ya kimisionari mwishoni mwa wiki.

Masista wa jumuiya mpya wanasubiri kwa shauku mkutano ujao ambao utafanyika kwenye makao yajayo ya Novisiati hapo Sant’ Agnese, Nomentana.

***Sr. Joan Stoverink, ASC***







Jumuiya ya malezi inaonekana hapa:
nyuma:
***Sr. Emanuela Škarica, Sr. Martha Joseph, Sr. Marisa Nardoni***
walioketi ni:
***Sr. Joan Stoverink, Sr. Mariamma Kunnackal***









Eneo la Bara: Africa
Mission Liberia

## Yaliyoko sasa Liberia

Msimu wa mvua unaendelea hapa kwa joto la chini wakati huko Marekani wanaendelea kuhangaika kupumua na kutoka jasho. Wiki hii, safari ya kwenda kijiji cha Pleebo ni kwa mwendo wa saa tatu, ambapo kawaida huwa ni masaa mawili, hii inathibitisha kwa nini safari ni chache wakati wa msimu wa mvua. Ni gari la gurudumu nne tu ndilo limeturuhusu tukae barabarani na kupanda milima miwili. Kulikuwa na watu ambao hawakutambua na ambao, walikwama, walihitaji kuondolewa kwenye matope ya udongo mwekundu. Asante Mungu tumesafari salama bila kupata ajali.

Mwezi uliopita, huko Gran Cess, utaratibu wa maisha ya kila siku uliingiliwa na kundi la wachimbaji madini kutoka Nigeria, ambao walikuja kuandaa kazi ya uchimbaji wa madini ya dhahabu kando ya bonde la mto. Zana zao sasa ziko mbele ya nyumba ya meya na wachimba madini wa Nigeria wamerudi nyumbani, ushindi wa uhakika wa mazingira kwa wakazi wengi, walikuwa na wasiwasi kwa sababu walijua kuwa kazi hii ingeathiri maji na kuharibu uvuvi na upatikanaji wa kaa, chakula muhimu kwa wakazi wa eneo hilo.

Hali hii ilitokeaje? Grand Cess imegawanywa katika jamii tisa pamoja na jamii ya kikabila ya historia ndefu na mila. Kila jamii huteua mtu anayeiwakilisha kwenye baraza la kijiji. Mkuu wa kabila ni yule anayewawakilisha kwenye baraza.

Inaonekana kwamba kiongozi wa kabila moja aliamua kuuza sehemu ya mali iliyomo mtoni kwa kampuni ya Nigeria bila kuwajulisha au kujadiliana na viongozi wengine. Jamii kwa ujumla ilitambua wakati vifaa vilipofika, na mara moja baadhi ya watu walianza kutoa taarifa na kuandaa pingamizi kwa upande wa wenyeji. Kulikuwa na maandamano na matembezi. Hatimaye, wakati wa maandamano kwenye bonde la mto, Wapingaji walikamata mashine na vifaa (vya chuma nzito) waliisukuma hadi mbele ya nyumba ya meya (picha).





Bila shaka, hii ilimuudhi sana mkuu wa kabila. Kulikuwa na mazungumzo na, neno la Meya, "tumepatana". Muda utafunua matunda ya mchakato huu wa upatanisho ikiwa katika kijiji hiki cha wenyeji 2,000 maelewano yatabaki, hasa kwa sababu mji wa jirani umeruhusu kampuni ya madini kubaki. Wakati wa safari kutoka Monrovia, katika vijiji viwili vidogo niliona ishara kubwa za uharibifu wa mazingira na uchafuzi unaosababishwa na migodi ya dhahabu. Asante Mungu, baadhi ya wananchi wa kijiji, vijana na wazee, wanaelewa kuhusu uharibifu ambao uchimbajii huu ungesababisha kwenye mazingira ya asili.

Nikibadili mada: kuanzia tarehe 3 Septemba mwaka mpya wa masomo ulianza. Shule ya Mt. Patrick itakuwa mwenyeji wa wanafunzi 350 kutoka shule ya chekechea hadi daraja la tisa. Pia kuna shule mbili za umma, shule ya msingi na shule ya kati / sekondari katika jengo moja. Kuna pia shule moja ya chekechea binafsi. Sr. Therese atafundisha Kiingereza darasa la 7 na dini kwa watoto kutoka darasa la 7 hadi 9. Kwa nyongeza, kama shughuli baada ya masaa ya shule, ataunda kikundi cha wasichana kuendana na umri, kwa ajili ya maendeleo ya jumla kupitia shughuli zinazoendana na umri. Sr. Therese anatarajia kufanya kazi na chama cha kujitolea cha Peace Corps ambacho hufundisha katika shule ya sekondari ya umma, ili kufungua shughuli hii kwa wasichana wote wa Grand Cess.

Wakati huo huo, Sr. Zita anaendelea kufanya kazi ili kuandaa chumba kwa ajili ya shule ya ushonaji. Anafanya kazi na baadhi ya wanawake ambao walijifunza shughuli hii kwenye miaka ya 80 wakati alipokuwa hapa. Shughuli mpya kwa ajili yake (na kwa ajili ya parokia) itakuwa kukutana na watoto wadogo, wakati wa Misa ya Jumapili, nje ya kanisa, wakati wa mahubiri (mara kwa mara dakika 45 kwa ajili ya tafsiri kwa lugha ya Kru) ili kuelezea ujumbe ya injili kuifanya kuwa na maana kwao. Sr. Zita pia ametengeneza bustani na kupanda miti (mitende na matunda) na mananasi.

Furahieni, msimu wa vuli ambao hapa haupo.

***Sr. Therese Wetta, ASC***

# Semina: Maisha ya jumuiya ASC





Padre George, CPPS pamoja na juniors watatu ambao walifanya upya ahadi, Sr. Magdalena George Chipanta, Sr. Maria Elias Malele na Sr. Rosemary Elias Malele



Kuanzia tarehe 10 hadi 14 Septemba 2018 huko Morogoro ilifanyika semina kwa ajili ya masista vijana ASC, ambayo iliongozwa na Padre Georgi Mwaluko, CPPS; mada ya semina ilikuwa ni Maisha ya jumuiya kulingana na karama ASC.

Sisi Masista vijana ASC, kila mwaka, zaidi ya kushiriki semina zinazopangwa na Region, tunapata nafasi ya kushiriki semina na kozi zingine ili kukua zaidi kiroho. Kwa ajili ya hilo tunaushukuru uongozi wa Region kwa nafasi hii.

Padre George alizungumza juu ya maisha ya jumuiya ambayo ni sehemu muhimu sana kwa ajili ya ukuaji wetu, Yesu ni kiini cha maisha yetu ya pamoja na sisi kila mmoja anamhitaji mwingine kwa sababu kila mmoja ana vipaji tofauti. Jumuiya inajengwa katika msingi wa Neno la Mungu, sala na Ekaristi takatifu, upendo na upatanisho. Kila mmoja anaalikwa kutunza maisha ya jumuiya akishiriki kikamilifu katika ujenzi wake. Kila mmoja wetu ni mwajibikiji wa mipango na nyakati za mashirikisho. Jumuiya ni kwa ajili ya utume.

Yeye alitueleza kwamba utandawazi, unarahisisha mawasiliano, waweza kuwa msaada kwa ukuaji wa maisha ya jumuiya lakini wakati mwingine badala yake unakuwa ni njia ya uharibifu. Matumizi ya simu na komputa yanarahisisha mawasiliano, lakini mara pengine vyombo hivi vya mawasiliano vinapotumiwa vibaya huharibu mahusiano ya wanajumuiya, utume, sala ama mfumo mzima wa maisha ya jumuiya. Alituhimiza kuwa waangalifu katika utumiaji wa vyombo vya mawasiliano ili visiwe chanzo cha uharibifu kwa maisha ya jumuiya bali viongeze uhai wa maisha ya jumuiya, na kusaidia katika ukuji wake.

***Sr. Getruda Faustus Masebe, ASC na Sr. Imakulata Michael Sayumwe, ASC***

Eneo la Bara: Amerika
Fondation Argentina

# Wanafunzi wa Shule ya Damu Azizi

Wanafunzi wa darasa la 6° wa shule "Damu Azizi" (ARGENTINA), wakihamasishwa na mafundisho ya lugha ya Fiorella Fisicaro, walisoma na kufanyia kazi masimulizi ya mwandishi Norma Huidobro: Paka juu ya roshani, pete ya zumaridi kijani, mchuzi wenye sumu, haramia na mwanamke mcheza ngoma. Mwandishi aliwatembelea wanafunzi wakati wa kipindi cha somo na vijana walimwuliza maswali, na wote walijisikia kuhusishwa.
Bibi Norma aliwahamasisha wanafunzi kuendeleza tabia ya usomaji, ambayo ni mazoezi mazuri ya akili, yenye mambo mengi, yanahusisha mtiririko wa tabia ya utambuzi ambayo, wakati huo huo, inakua na kutajirishana wakati shughuli hii inakuwa endelevu. Kwa sababu hii, kazi ya kusoma daima iko kwenye elimu na katika maisha ya kila mtu. Ni uzoefu wa kibinafsi na usioweza kurudiwa, ambao hufuatiwa na mfululizo wa manufaa ya vitendo ambavyo tunaweza kuvifanya katika maisha yetu ya kila siku.





Wanafunzi wa tano wa madarasa ya A,B, C wa shule ileile, katika kipindi cha mwezi Septemba, waliandaa kampeni ya umoja wa kukusanya chakula cha watoto wa shule ya chekechea ya "Mt. Maria De Mattias". Mnamo Septemba 26 walienda "Jardin Patra" ili kupata chakula na kukutana na kucheza na watoto wa Kituo hicho.
Ilikuwa jioni yenye manufaa, kwa sababu vijana walijifunza thamani ya mshikamano. Sista Maria Elena Bilbao alifurahi sana kwa uwepo wa wanafunzi wa shule. Kama alivyokuwa akisema MDM: "Uwe na furaha na ufanye kazi kwa moyo kwa ajili ya upendo wa Yesu Kristo, uwapende sana wasichana"... barua 391 MDM.

***Sr. Susana Misermont, ASC***

# Kumkumbuka Rudy Torrini



Wiki iliyopita tulifahamu juu ya kifo cha mchonga sanamu maarufu wa St. Louis, Rodolfo "Rudy" Torrini, kilichotokea Jumatano Septemba 5 akiwa na umri wa miaka 95, kutokana na matatizo yaliyohusiana na shida za uzee.

Bwana Torrini, mwana wa mpiga chapa wa Kiitaliano mhamiaji na mpiga kinanda wa filamu za kimya kimya alikuwa anajulikana kwa sanamu zake ambazo leo zinapamba eneo la St Louis. Miongoni mwa kazi zake maarufu ni: mchezaji wa soka, afisa wa polisi, mvulana na mbwa wake, wahamiaji wa Italia, Dk. Martin Luther King Jr, Papa John Paul II na mtoto wa miaka 9 aliyeuawa kwa risasi.

Lakini cha muhimu kwa Waabuduo ni sanamu za Mashahidi watano wa Upendo katika bustani ya Nyumba ya Shirika ya Ruma, ambazo zinawakilisha wananwake katika mduara, walioshikamana mikono yao pamoja na nyuso zao zikiwa zimeangalia mbinguni kwa furaha.

Mtindo wa kawaida wa sanamu unaonyesha maisha yao ya kawaida nchini Liberia. Mchongaji aliwaweka katika mduara ili kuashiria umoja wao na "taji la kifodini chao". Aliandika hivi: "Tendo lao lilikuwa ni kielelezo cha zawadi kuu ya maisha yao, kipindi ambapo neno muhimu kwa wote ni lile la kushinda".

Sanamu, zilizowekwa wakfu tarehe 26 Juni mwaka 1994 ilikuwa ni nafasi kwa kushirikishana historia ya masista na wale ambao hawakuwafahamu. Kwetu sisi Waabuduo unabaki msukumo iwe ni maisha ya masista wetu, ama zawadi ya mchonga sanamu vinavyoshuhudia roho yao na utu wao licha ya huzuni.



***Sr. Barbara Jean Franklin, ASC***

# Sisi ni "kijiji" ni haki kulea watoto

Tarehe 30 Juni Sr. Jo Ann Mark aliopokea barua pepe kutoka shirika linalohudumia wahamiaji, lililo chini ya umoja wa wakuu wa mashirika ya kitawa ya USA (LCWR).

Barua pepe ilikuwa inaomba utayari wa jumuiya za kitawa kutoa nafasi ya shule ya chekechea inayoombwa. Baada ya kujadiliana juu ya ombi hili pamoja na timu ya uongozi, Sr. Jo Ann alifanya mawasiliano na waombaji akijishughulisha hadi mwisho, hivyo kuamua kuanzisha Kijiji ili kupokea familia zinazotafuta shule ya chekechea.

Ili kuanzisha kijiji kwenye Nyumba ya Shirika ya Wichita, ilitosha kuwa na nesi mmoja anayefanya kazi kwenye Caritas, kutoka Angola ambaye anaongea Kifaranza, Mwabuduo mmoja anayeongea Kireno na kikundi cha wafanyakazi ambao wanaongea Kihispania. Kuongeza wafanya wa usafi na wafanyakazi wengine wanaoshugulika na utafutaji wa mavazi na midoli ya kuchezea kuendana na umri na hivyo Nyumba ya Shirika iko tayari kujibadilisha katika kijiji ili kupokea familia mbili zinazotafuta shule ya chekechea.

Ni jumla ya watu tisa ambao sasa wanaishi kwenye chumba C cha gorofa ya tatu. Familia moja ya Frederico Julho na watoto wake wanne, Frederico (anayeitwa Fredlson), miaka 6; Madalena (anayeitwa Neydi), miaka 11; Mandala (anayeitwa Jonilson), miaka 4 na Fernanda, miaka 7.

Familia nyingine inaundwa na Helena Clementia na watoto wake watatu, Marian, miaka 9; Edwina, miaka 3; na Madalina, mwaka mmoja na nusu.

Mahali ambapo familia zimekaribishwa panabeba jina la Mwenye heri Stanley Rother ambaye picha inaonekana kwenye korido.

Frederico Julho kwa asili ni wa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, lakini amekaa miaka mingi huko Angola, mahali ambapo watoto wake walizaliwa na kukua.

Wakati wa ukimbizi huko Kongo, Federico na watoto walitengana na mke na watoto wao wawili wadogo zaidi. Miezi mitano ya mwisho, Federico alibaki kama mzazi mmoja ambaye kutoka Congo alifika USA, kwanza huko Dallas na baadaye hapa Wichita tarehe 17 Agosti.

Kwa msaada wa vituo kadhaa hapa Wichita, aliweza kufikia kiwango cha kumpata mke wake na tarehe 13 Agosti, yeye na watoto waliongea naye kwenye simu, na kugundua kuwa yeye na watoto wadogo zaidi walikuwa Ivory Coast. Changamoto sasa ni kupata namna ya kuiunganisha familia.

Masista wengi wanaamini kuwa ilikuwa ni kwa maombezi ya Pd. Stan (na Msalaba Mwekundu wa Kimataifa) kwamba mke wake na watoto wake waliweza kupatikana.

Watoto watatu wakubwa zaidi wa Frederico wanaenda shule ambapo yule mdogo zaidi anaenda shule ya chekechea. Baada ya, kama wiki mbili zilizopita, tulipokea familia ya Clementia. Masista kadhaa wanawaandaa watoto kwa ajili ya shule, kwa ajili ya mpango "Head Start" na wanawafundisha lugha ya Kiingereza.

Masista wa kijiji wanafanya kwa namna zote wanazoweza ilikusaidia familia zote mbili.

Wao hutoa usafiri wa watoto kwenda shule ya chekechea na shule nyingine wakati mabasi hayafanyi kazi, huwasaidia kufanya mazoezi yao ya nyumbani, kuwafundisha Kiingereza kwa njia ya michezo ya Dominos na Old Maid na kuwaangalia wakati wanaendesha baiskeli. Hata watu wazima hutoa masomo ya Kiingereza na kuwa tayari kuwasindikiza ikiwa kuna haja kwenye mashirika mbalimbali.

Wafanyakazi wa Kituo wametusaidia kutambua mahitaji yao na mojawapo ya vipaumbele kwa wasichana ni kutengeneza nywele zao kulingana na mtindo wa kiafrika. Wasichana watatu wakubwa wanajisikia kuheshimika zaidi sasa kwa kuwa nywele zao zinachanwa vizuri.

Sasa vyombo vya usafiri vya Kituo vina nafasi kubwa ya maegesho (ukubwa tofauti unahitajika kuendana na umri tofauti wa watoto) na chumba kikuu cha chakula kina viti viwili vya juu. Edwina anatumia kitanda cha mtoto tulichopewa.

Tangu watoto walipopata makazi wamependeza. Wafanyakazi wa Kituo wanaendelea kusaidia katika kutafsiri na kuwasaidia watoto kwa umakini.

***Sr. Diana Rawlings, ASC***






Eneo la Bara: Ulaya
Region Italia

## …Ndani ya Nchi ya Argentina





Majira ya baridi ya Argentina yalinikaribisha kwa upendo wa ukumbatio na wa moyo wa masista Patricia Ataria, Ana Maria Krall, Marcela Cravera, Maria Mossa, Maria Elena Bilbao, Miriam Ortiz, na Susana Misermont.
Mudawafamilianaudugu,siowatukio.Utambuzimpya wa tunu zilizojengwa pamoja, kama kumbukumbu na masimulizi, umetuunda na kutujengea katika furaha ya kujiona dada na marafiki. Tumeishi muda mwingi wa kazi na uwajibikaji ambapo tulisoma, tulifanya uhakiki na kufanya uchambuzi juu ya maisha yetu kama wanawake waliowekwa wakfu katika ishara ya damu ndani ya Kanisa la ulimwengu na hasa hapa Argentina. Siku za kutosha na za furaha zilizosaidiwa na mchango wenye manufaa kutoka kwa wote. Mada mbili kwa kina: tunasoma tena "ufuasi wa Kristo" kama wito wa pekee kwa ajili yangu, kwa ishara ya udugu tunayoiishi kwa pamoja; tunajiweka wenyewe katika uchambuzi juu ya hali na maisha ya Foundation ASC Argentina ndani ya Kanisa leo.
Mashirikisho aminifu na yenye utajiri wa mapenzi mema ya wote yametuwezesha kupata miongozo kwa ajili ya kusonga mbele kuelekea siku zijazo.
Sala na Misa Takatifu, zilizoadhimishwa kwa unyenyekevu katika maombi yasiyokoma kwa Roho Mtakatifu, yalisaidia na kutia nguvu uchambuzi. Kisha kuzama katika utume wa masista Argentina: kazi za kichungaji katika maeneo yote; kuwa pamoja na walio wa mwisho; kukuza hali ya maskini miongoni mwa maskini; ya wale wenye matatizo makubwa ya kijamii. Ni Kanisa la Papa Francis ambalo linajionesha kwangu kama msafara ambao mikono inanyoshwa ili kusaidiana katika mkono wa huruma ya umoja, kama katika safari ya hija takatifu. Baada ya kutembea kwa muda mrefu kwenye barabara zenye mashimo na matope kati ya nyumba mbovu, ninaalikwa kwenye jengo ambalo linaandaliwa na jumuiya nzima ya parokia ambayo inatoa huduma ya kichungaji kwenye Villas. Watu wanataka kuniambia, na wanasema, kwa ushiriki hai ambapo las hermanas ni baraka, ni mkono na tabasamu ya Mungu kwao. Pia ninastaajabia uhuishaji wa malezi katika kituo cha elimu huko Villa Bosch ambacho kina idadi ya mahudhurio 1,500 kati ya watoto wadogo, wakubwa na vijana. Hugusa mfumo mzima wa elimu unaoambatana vema na karama ya Damu ya Kristo. Utafiti wa kisayansi na utumishi wa upendo vinashikamana ajabu. Na ... katika hitimisho la kukaa Argentina, kama furaha na matumaini, vijana wawili wanatokea: Mimi ninazungumza nao kwa muda mrefu kuhusu wito wa pekee ambao unaweza kusikika ndani ya moyo. Kwenye ndege ya kurudi kwenda Italia nimeweka kila kitu ndani ya moyo wangu na kukabidhi kila ahadi kwa Mungu. Asanteni masista kwa maisha yenu ya kujitoa kwa Kristo kwa ajili ya watu katika ishara ya Damu ya Azizi!

**_Sr. Nicla Spezzati, ASC_**
*Mkuu wa Region*

Region Italia



## Majira ya uchambuzi

Tarehe 6 - 10 Agosti 2018 muda mzuri ambapo wewe kijana katika uchambuzi wa wito umetaka kuutenga "likizo katika Roho". San Vito Romano (RM) eneo kwa ajili ya mang'amuzi ya kufahamiana katika utafiti wa pamoja juu ya mapenzi ya Mungu. Kwenye kikundi cha wasichana ambao tayari wameanza safari huenda wakaongezeka wapya. Kuna sababu ya kumshukuru Bwana na kumwomba neema ya kuendelea kushuhudia furaha ambayo Yeye ndiye chanzo! Chukua moyo wako mikononi mwako! Kauli mbiu iliyopamba mawazo ya utafiti, siku zetu tulizoziishi katika mzunguko wa zamu za muda kwenye chumba na nyakati za kutoka ambazo zilisaidia kupumzisha mwili na kuelekeza moyo juu. Mnamo tarehe 11 na 12, hapa katikati ya umati wa Circo Massimo pamoja na vijana wengi wa Italia ambao, wakiwa safarini kutoka pande zote, wamekabiliana na joto la majira ya joto ili kuongea na Papa Francis kwamba ndoto zao zinapaswa kulindwa na kutetewa. Mang'amuzi yenye nguvu yalikamilika kwenye Kiwanja cha Mt. Pietro ili ... kurudi tena ulimwenguni!!





**_Sr. Miriam De Michele, ASC_**

# Kugusa madonda ya Yesu



Uanzishaji wa uinjilishaji wa kipolandi Kituo cha Yesu unaambatana na tamasha la muziki wa Poland-Rock (Woodstock ya zamani) ambalo limekuwa likifanyika tangu 1999. Wakati wa Kituo cha Yesu, zaidi ya matukio ya muziki, yaliyoandaliwa, kulikuwa pia na ritiriti, mikutano na warsha kwa ajili wainjilishaji na kwa ajili ya wote waliopenda.

Kituo cha Yesu ni sehemu ya sanaa hii kubwa na ni nzuri kwa sababu washiriki, pamoja na uwepo wao, wanakumbuka kwamba Yesu hatengi mtu yeyote.

Katika mashamba ya Woodstock nilionja kilio kikubwa cha Damu ya Kristo. Yesu haniiti tu kutoa muda wangu kwa jirani aliyepotea na kutangaza Habari yake Njema, bali pia kumruhusu abadilishe moyo wangu kupitia kukutana na watu tofauti. Kwenye Kituo cha Yesu, mtu anaweza kumwona Yesu kama Injili ambayo inabadilisha maisha na kuyapa maana.

Nikitembea kwenye barabara za jiji hili lisilofikiriwa lenye mahema, nilivutiwa na watu waliokuwa wakiweka kambi marundo ya takataka. Wakati tunatembe kama kikundi, mmoja wa wainjilishaji alitufanya tuwe makini kwa mtu ambaye alikuwa amesongomezwa kwenye karatasi ngumu karibu na rundo la makopo ya bia. Mara ya kwanza ilikuwa inaonekana kama alikuwa na umri karibu miaka 60, ameharibika kama ilivyokuwa kwa pombe na hata zaidi kwa upweke. Kwa uhalisiai alikuwa na umri wa miaka 38 na alikuwa na ndoto ya kuwa na familia. Watu hawa walio peke yao wanaokuja kutoka Woodstock ili waweze kusahau matatizo yao na kujizamisha katika pombe, mara nyingi huwageukia wainjilishaji ili waweze kuzungumza. Hapa ni hadithi ya Daudi: niilikuwa na nafuu zaidi miaka miwili iliyopita. Leo makovu na chale kwenye ngozi husema zaidi kuliko maneno yake yasiyo na mpangilio. Mwaliko wao kuja kwenye upendo umekuwa kwangu kilio cha Yesu, cha Damu Yake.

Kati ya umati uliochafuka kwa vumbi lenye rangi ya Krishna, mtu anaweza kuanguka katika udanganyifu kwamba huu ni uhuru! Hii ni usawa na udugu! Hata hivyo, vumbi jekundu la kambi ya Kostrzyn lilinikumbusha mfululizo msichana ambaye alikuwa akilia kwenye mikono yetu asubuhi alidanganyika kwa wazo la aina hii ya uhuru. Majeraha ya kibinadamu mara nyingi hujificha nyuma ya sura kutokuwa makini na kwenye uhuru wa kimapenzi. Kila siku nilijifunza kutambua katika matukio haya kilio cha kukata tamaa ya upendo, bado ninamkumbuka mvulana aliyekuwa na nywele za kijani, msanii wa "kufanya-mwenyewe", ambaye baada ya dakika chache alituambia kuwa aliteseka kutokana na msongo wa mawazo kwa miaka mingi na kwamba sikukuu ilikuwa ni njia ya kusahau kila kitu, ili kujiondoa mwenyewe kutoka kwenye mawazo yake. Nilivutiwa sana na mtazamo wa mpenzi wake ambaye kwa uvumilivu mkubwa alikuwa akisubiri kurudi kwake, atakapokuwa amekomaa na kuwa tayari kujenga familia.

Kwangu mimi pia inanihusu kuchukua majeraha ya mtu mwingine, udhaifu wa Kanisa, nguvu ya Kristo; lakini pia inakabiliana na ukweli kwamba Kanisa, kama taasisi, huumiza wengine na kwamba sisi, watu wa Kanisa, pia ni sababu ya kashfa na kwa sababu hii wengi wanamwacha Mungu.

Nakumbuka hasa mkutano na kikundi cha watu chni ya hema. Bila haraka, wote walijitambulisha, walizungumza kuhusu familia zao. Marafiki zetu walilalamika kuhusu Kanisa, walizungumzia juu ya kuacha imani. Mazungumzo yetu yamekuwa ya kina zaidi, tumegusa juu ya mada makubwa zaidi. Jambo muhimu sana lilikuwa sala ya pamoja ya maombi. Kuondoka katika kikundi hiki tulihisi kutajirishana sisi wenyewe na kutajirishwa na Mungu. Uzoefu wa siku hizi ulinionyeshe uso wa Pasaka wa Kanisa kwa sababu Kristo huchukua mateso yetu, hatendi tofauti kati ya "wazuri" wa Kituo cha Yesu na wale "wabaya" wa Poland -Rock. Anatuunganisha katika Damu yake na anatuonyesha kwamba tunahitajiana kila mmoja.

Ninalipenda sana na Kanisa hili chini ya hema: limeonekana kama hospitali ya shamba ambayo inatoa mahali salama pa kuishi. Mbele ya duka kubwa, Lidl, daima limejaa watu, tukirudi kutoka kwenye uinjilishaji, tuliweza kuona watu waliokuwa chini wakiwa wamechoka na wakiwa wamelewa au familia pamoja na watoto zilikuja kushangaa, wakati mapadri wakiungamisha karibu na hema na kusali pamoja nawalei na watu waliowekwa wakfu. Ninalipenda sana Kanisa hili ambalo linatoka kwenda linakutana na mtu huyo, linamtafuta, linamkumbatia na kumtangazia Yesu.Nina hamu ya Kanisa hili kwa sababu ni hai hata kama aomba kuthubutu. Ni la kujihatarisha, lakini hatuna Kanisa lingine.



***Sr. Tatiana Studentowa, ASC***

# Kusherehekea kipindi cha uumbaji kwa mtindo wa ASC

*"Namshukuru Mungu kwa zawadi ya nyumba yetu ya pamoja na wote wale wenye mapenzi mema wanaojishughulisha kuilinda."*

*Papa Francesco, 1 Septemba 2018*

Kuanzia tarehe 1 Septemba, siku ya sala kwa ajili ya uumbaji, mpaka tarehe 4 Oktoba , siku ya sikukuu ya Mtakatifu Francisco, mlinzi mtakatifu wa ikolojia ya mapokeo katika mila nyingi, wakati maalum uliadhimishwa ili kumtukuza Muumba na kulinda zawadi ya uumbaji. *Msimu wa uumbaji*, ulianzishwa mnamo 1989 na Kanisa la Orthodox, sasa umekubaliwa na familia kubwa ya umoja wa kidini ambayo hukutana ili kusali, kutunza uumbaji na kukabiliana na mwito wa haraka ili kupata suluhisho la shida za nyumba yetu ya pamoja.



Sisi Waabuduo wameitikia mwaliko na tumeungana na Wakristo wa ulimwengu wote ambao wamesali na kusherehekea, wakati tunafanya kazi yetu uongozi wa uumbaji wa Mungu. Na hapa tunashirikisha baadhi ya historia zetu ...



Sr. Lisbeth alishirikisha kwamba masista wetu huko *Schaan*, pamoja na wanaparokia wengine, walifanya mang'amuzi ya sala, wakiongozwa na m sakristia wa Kanisa mahalia; wakizama katika mazingira kwa mwonekano mzuri juu ya milima na kwenye ziwa, "ili kufanya kufahamu zaidi uzuri wa asili ambamo tunaishi kila siku, wakati tukitafakari juu ya mahusiano ya upendo kwa viumbe vyote, alitualika kuwa watu wenye shukrani na waangalifu. " Hata masista wetu huko *Marekani* waliungana na sala ya Papa Francisco "sala ya Kikiristo ya Muungano pamoja na Viumbe" kwa mwezi mzima, na sala ya Idara (North-South-East-West), na kuombea baraka idara zote ulimwenguni. Mwisho wa kipindi, Sr. Anne Irose wakati wa sherehe, kushika kote mikononi mwake ramani ya dunia aliongoza maandamano nje ya Kanisa la Ruma, alitualika kutazama uumbaji ili kumwabudu na kumtukuza Mungu kwa ajili ya ardhi ambayo ni takatifu..



Huko **Zagreb**, Sr. Cecilija, anayehusika na mawasiliano ya JPIC / Vivat, aliandaai huduma sala ambayo ilitumika kwenye Region nzima na kuhawamasisha kuwahimiza masista wote "kuandaa shughuli mbalimbali na watoto, washirika na kwenye parokia ambapo wanatoa huduma zao." Huko **Hispania**, masista wetu waliungana na Wakatoliki na Waorthodox kwenye mkutano tafakari na sala iliyoandaliwa na Askofu Mkuu wa Madrid na kwenye Mkutano wa umoja wa Kanisa la Orthodox ambalo lilijumuisha hotuba juu ya Utunzaji wa Hewa, maonyesho ya hali ya hewa na huduma ya sala ya umoja wa makanisa. **Kwenye Nyumba ya Kuu**, jumuiya ya kimataifa ikiongozwa na Sr. Rani Padayattil ilikuwa na muda wa sala ya tafakari ya sala ambayo ilijumuisha kipindi cha mpito "kutoka kwenye tafakari hadi kwenye tendo" na hivyo kila sista aliandika tendo lake halisi kwa ajili ya utunzaji wa dunia. Nyajibu zilizoandikwa, baada ya kushirikishwa kwa sauti, zilibandikwa kwenye ubao "ili kila siku zitukumbushe kujitolea kwetu kwa uumbaji wa Mungu". Huko Roma, masista pia walishiriki katika Misa ya Laudato Si, iliyoadhimishwa kwenye bustani nzuri, iliyozungukwa na maajabu ya uumbaji. Na huko **Poland**, masista wetu wamesukumwa kuingia kwa undani kwenye mada na matatizo ya mazingira wakati huu ambapo nchi inajiandaa kwa ajili ya mkutano wa kimataifa wa hali ya hewa utakaofanyika huko Katowice Desemba. Tukio hili limewasukuma masista "kupitisha kanuni tatu husika na maisha ya kila siku: kutenganisha taka, kuokoa umeme na maji na kutumia tu mifuko ya karatasi au kitambaa wanaponunua vitu." Mfano wa jinsi ASCs walivyounganisha tunu za uumbaji na maisha ya kila siku!

Na tunajua kwamba bado kuna mipango mingi ambayo inafanyika kwa ajili ya uumbaji katika ulimwengu wa ASC na tunataka kukumbuka kwamba kila hatua iliyochukuliwa katika mwelekeo huu inaweza kufungua mioyo yetu ili kutufanya zaidi "makini kwa kilio cha Damu".









***Sr. Dani Brought, ASC***

## Kalenda ya Uongozi Mkuu




**21 - 30 Novemba** Mktano wa Halmashauri Kuu Iliyopanuka 2018

## Sikukuu za kuzaliwa: Tunashrehekea maisha ya



| | | |
|---|---|---|
| Miaka 50 | | |
| **Sr. Analice Pereira Vieira** | 25/11/1968 | Manaus |
| Miaka 60 | | |
| **Sr. Tatyana Ugaynova** | 05/11/ 1958 | Wrozław |
| **Sr. Angela Maria Pinho Cavalcante** | 24/11/1958 | Manaus |
| **Sr. Eun Sook Cecilia Kim** | 30/11/1958 | Korea |
| Miaka 80 | | |
| **Sr. Maria Grazia Carpenito** | 15/11/1938 | Italia |
| Miaka 90 | | |
| **Sr. Maria Iannotti** | 19/11/1928 | Italia |



## Waliorudi Nyumbani kwa Baba

| | | |
|---|---|---|
| 26/09/2018 | **Sr. Tommasina Siddi** | Italia |
| 21/10/2018 | **Sr. Silvina Pellegrini** | Italia |
| 28/10/2018 | **Sr. Esmeralda Gonçalves do Vale** | Manaus |





**Habiri ya kila mwezi**

*na*

***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI, N. 12, Novemba 2018**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Mimma Scalera, ASC**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Lisbeth Reichlin*** *- Kijerumani*